PRESS RELEASE

PR23/50

# Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Lafikia Makubaliano ya Ngazi ya Wafanyakazi na Serikali Kuhusu Mapitio ya Kwanza ya Mpango wa Ukopeshaji wa ECF (Extended Credit Facility) na Kukamirisha Majadiliano kwa Mwaka 2023 Chini ya Kanuni ya Nne ya Mkataba Ulioanzisha Shirika hilo (Article IV Consultation)

**FOR IMMEDIATE RELEASE**

End-of-Mission press releases include statements of IMF staff teams that convey preliminary findings after a visit to a country. The views expressed in this statement are those of the IMF staff and do not necessarily represent the views of the IMF's Executive Board. Based on the preliminary findings of this mission, staff will prepare a report that, subject to management approval, will be presented to the IMF's Executive Board for discussion and decision.

- *Mpango wa mageuzi wa serikali unalenga kuimarisha ufufuaji wa uchumi, kuhifadhi uthabiti wa uchumi, na kusaidia mageuzi ya kimuundo ili kuleta ukuaji wa uchumi endelevu na shirikishi*
- *Hatua muhimu za kisera za mpango wa mageuzi zinalenga katika kuimarisha nafasi katika bajeti ili kuruhusu matumizi yanayohitajika sana katika huduma za kijamii na uwekezaji wa umma kwenye miradi inayolipa zaidi, kuendeleza mageuzi ya kimuundo ili kuleta mazingira wezeshi ya uwekezaji na kutengeneza nafasi za ajira, na kuifanya sera ya fedha kuwa ya kisasa na usimamizi wa fedha ili kuhifadhi uthabiti wa mfumo wa kifedha, na kukuza ukuaji wa kifedha.*
- *Makubaliano haya ya awali kati ya wafanyakazi wa IMF na serikali yatategemea idhini ya uongozi shirika na Bodi Tendaji yake.*

**Washington, DC**: Timu ya wafanyakazi kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) wakiongozwa na Charalambos Tsangarides walifanya vikao vya majadiliano mjini Dodoma na Dar es Salaam kuanzia tarehe Februari 8 hadi Februari 23, 2023, ili kujadili maendeleo ya utekelezaji wa mpango wa mageuzi na vipaumbele vya sera za serikali katika muktadha wa mapitio ya kwanza ya mpango wake wa ukopeshaji wa muda wa miezi 40 wa ECF (Extended Credit Facility) kwa Tanzania. Mpango huu uliidhinishwa kwa jumla ya kiasi cha SDR 795.58 milioni (dola za Marekani bilioni 1.046 wakati huo) mnamo mwezi Julai 18, 2022. Timu ya wafanyakazi pia ilifanya mashauriano ya mwaka 2023 chini ya kanuni ya nne ya mkataba ulionzisha IMF (Article IV Consultation).Mwishoni mwa ziara yake, Bwana Tsangarides, alitoa taarifa ifuatayo:

"Tanzania na timu ya wafanyakazi wa IMF wamefikia makubaliano ya ngazi ya wafanyakazi kuhusu mapitio ya kwanza ya mpango wa ukopeshaji wa muda wa miezi 40 chini ya mpango ECF (Extended Credit Facility). Makubaliano ya ngazi ya wafanyakazi yatategemea kuidhinishwa na uongozi na Bodi Tendaji ya IMF wiki zijazo. Tanzania itapatiwa kiasi cha SDR 113.37 milioni (sawa na dola za Marekani milioni 151) baada ya kukamilika kwa mapitio ya

Bodi Tendaji ya IMF na hivyo kufikisha jumla ya SDR 228.73 milioni (sawa na dola za marekani milioni 302.7) msaada wa kifedha kutoka IMF chini ya mpango huu.

"Uchumi wa Tanzania unaendelea kuimarika kutokana na athari za janga la UVIKO-19 licha ya changamoto zinazotokana na mwenendo wa uchumi wa dunia. Wakati baadhi ya sekta zikiwemo madini, utalii, na huduma nyingine zikionyesha kuimarika katika mwaka 2022, ukuaji wa uchumi kwa mwaka huo unakadiriwa kufikia hadi asilimia 4.7, hali inayoakisi athari za hali ya uchumi wa dunia, na athari za uhaba wa mvua kwenye uzalishaji wa umeme na kilimo. Licha ya ruzuku zilizotolewa na serikali kwenye bei za mafuta na mbolea, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 4.9 (mwaka hadi mwaka) mwezi Januari (kutoka asilimia 4.0 mwaka uliopita), ukikaribia kiwango cha juu cha asilimia 5 cha Benki Kuu ya Tanzania. Pamoja na mfumuko wa bei kupanda, Benki Kuu ya Tanzania imeongeza mauzo ya dhamana za serikali za muda mfupi ili kupunguza ukwasi uliozidi kwenye uchumi.

"Uchumi unanufaika kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara, lakini pia unatarajiwa kuendelea kukabiliwa na athari ya vita inayoendelea nchini Ukraine. Ukuaji wa uchumi mwaka 2023 unatarajiwa kuwa asilimia 5.2 na mfumuko wa bei kuvuka lengo la Benki Kuu ya Tanzania na kufikia takriban asilimia 5.3 ifikapo mwishoni wa mwaka huu wa fedha. Nakisi ya ulali wa bidhaa na huduma za nje inakadiriwa kubaki juu katika mwaka 2023 kutokana na hali ya wasiwasi kwenye uchumi wa dunia.

"Katika muktadha wa ukuaji wa wastani wa mapato, ongezeko kwenye matumizi ya huduma za kijamii linapewa kipaumbele kutokana na kuhamisha fedha kutoka kwenye baadhi ya miradi ya maendeleo kwenda kwenye huduma za kijamii, bila kubadili msimamo wa sera ya mapato na matumizi ya serikali kulingana na malengo ya mpango wa ECF. Kutokana na kupata fedha kidogo kutoka nje, nakisi ya bajeti iligharimiwa kwa kiasi kikubwa na fedha zilizokopwa kutoka vyanzo vya ndani. Kasi ya uhakiki wa madeni ya ndani ya serikali ulipungua na kuwa nyuma ya malengo ya serikali.

"Benki Kuu ya Tanzania inategemea zaidi mauzo ya fedha za kigeni kwa ajili ya kukabiliana na misukosuko kutoka nje. Tangu mwaka jana Shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa tulivu dhidi ya dola ya Marekani, ikishuka thamani kwa asilimia 0.6 tu (mwaka hadi mwaka) hadi mwisho wa mwaka 2022. Wakati huo, fahilisi halisi ya ubadilishaji fedha kati ya shilingi na sarafu za nchi washirika wa biashara ilipanda kwa takriban asilimia 3.7 (mwaka hadi mwaka) hadi mwisho wa Desemba 2022. Kiwango cha akiba ya fedha za kigeni katika mwaka wa kalenda wa 2022 kilipungua kwa dola za Marekani bilioni 1.2 na kufikia dola bilioni 5.2 (sawa na takriban miezi 4.3 ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje) katika mwezi wa Desemba 2022.

"Katika muda wa ujao, usaidizi wa muda wa kifedha kwenye uchumi unapaswa kuendelea ili kukinga uchumi kutokana na athari za vita nchini Ukraine. Sera ya fedha itaendelea kuelekezwa kwa kuzingatia mfumuko halisi wa bei na unaotarajiwa, huku ikiruhusu viwango vya ubadilishaji wa fedha kuendana na uhalisia ili kulinda uchumi dhidi ya athari za kiuchumi kutoka nje ya nchi.

"Kama ajenda zilizopo kwenye mpango wa mageuzi ya kimuundo zitatekelezwa ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira bora ya biashara na kuimarisha utawala bora, ukuaji halisi wa Pato la Taifa unatarajiwa kurudi kwa takriban asilimia 7 katika kipindi cha muda wa kati, mfumuko wa bei unatarajiwa kurejea kwenye lengo la Benki Kuu ya Tanzania, na nakisi ya ulali wa bidhaa na huduma za nje kupungua kwa wastani katika muda wa kati wakati athari kwenye uchumi wa dunia zikipungua na mageuzi yatakapoanza kuonyesha mafanikio. Juhudi za kukusanya mapato pamoja na juhudi za sera ya mapato na matumizi ya serikali

zinatarajiwa kuboresha bajeti ya serikali huko mbeleni. Kuboresha mfumo wa sera ya fedha kwa kuhamia kwenye mfumo wa sera ya fedha inayotegemea viwango vya riba kutaboresha ufanisi wa sera ya fedha, huku kuboresha mfumo wa usimamizi wa fedha kunaweza kukuza uthabiti na kuimarika kwa sekta ya fedha. Kuendeleza mageuzi ya kimuundo kutaweka mazingira wezeshi kwa ukuaji endelevu na shirikishi ukiongozwa na sekta binafsi.

"Ujumbe wa wataalam kutoka IMF ulikutana na Waziri wa Fedha na Mipango Mwigulu Nchemba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania Emmanuel Tutuba, viongozi wengine waandamizi wa serikali, washirika wa maendeleo, na wawakilishi wa sekta binafsi. Ujumbe wa wataalam kutoka IMF unatoa shukrani kwa mamlaka za Tanzania kwa ushirikiano wao, ukarimu, na majadiliano yenye tija."